KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
DAYOSISI YA KASKAZINI MAGHARIBI
CHUO CHA MAFUNZO YA KILIMO NA MIFUGO IGABIRO
S.L.P 212-MULEBA
Simu: 0766382091/0620177959/0754756028
Barua pepe: igabirotia@yahoo.com Tovuti: www.igabirotia.ac.tz

Tarehe: ……..

Bw/Bi: **……**

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA CHUO CHA MAFUNZO YA KILIMO NA MIFUGO IGABIRO KWA NGAZI YA STASHAHADA MWAKA WA MASOMO 2020/2021

FANI YA STASHAHADA YA KILIMO MSETO (DIPLOMA IN GENERAL AGRICULTURE)

Husika na somo lililopo hapo juu.

Chuo cha mafunzo ya Kilimo na Mifugo **Igabiro** kipo wilayani Muleba – Kagera. Kutoka Muleba mjini ni Kilometa 15 magharibi ukipitia barabara ya Nshamba. Na kutoka Nshamba kufika chuoni ni kilometa 3 kusini mwa Nshamba barabara ya kwenda Kabale upande wa kushoto kuna kibao kinachoonesha chuo kilipo.Chuo kinamilikiwa na **Kanisa La Kiinjili La Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Magharibi.**

Chuo kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) tangu mwaka 2014 kwa usajili wa namba **(Cert.No.REG/ANE/018)**, Pia chuo kina ithibati.

NACTE pamoja na uongozi wa chuo cha mafunzo ya Kilimo na Mifugo **Igabiro** wanakupatia nafasi ya kupata mafunzo kwa ngazi ya **STASHAHADA ya kilimo mseto (Diploma in General Agriculture)** kwa muda wa mwaka mmoja**.**

Chuo kitafunguliwa tarehe 2 Novemba, 2020 na masomo yataanza lasimi tarehe 16 Novemba, 2020.

Chuo kinapokea wanachuo wa kutwa na bweni.

- **WANACHUO WA KUTWA**

Gharama za **mafunzo** kwa mwaka ni shilingi **Milioni moja tu** (**1,000,000/=**), ambazo utazilipa kwa vipindi vitatu.

1. Malipo wakati wa kuripoti chuoni ni Tsh **500,000/=**
2. Malipo awamu ya pili (Januari) ni Tsh **250,000/=**
3. Malipo awamu ya tatu (Aprili) ni Tsh **250,000/=**

- **WANACHUO WA BWENI**

Gharama za **mafunzo, bweni, chakula** na **matibabu** kwa mwaka ni **Milioni moja na laki nane tu** (**1,800,000/=**), ambazo utazilipa kwa vipindi vitatu.

1. Malipo wakati wa kuripoti chuoni ni Tsh **900,000/=**
2. Malipo awamu ya pili (Januari) ni Tsh **450,000/=**
3. Malipo awamu ya tatu (Aprili) ni Tsh **450,000/=**

NB: Vifaa na michango inayohitajika wakati wa usajili wa mwanachuo wa kutwa au bweni mara afikapo chuoni ni kama ifuatavyo;

i. Pasport size nne (4)
ii. Ream paper mbili (2) A4.

iii. Cheti cha kidato cha nne, sita na cheti cha kumaliza ASTASHAHADA.
iv. Cheti cha kuzaliwa (Birth certificate)
v. Cheti cha daktari (Medical certificate of fitness) fomu imeambatanishwa.
vi. Spring file mbili (02)
vii. Fedha kiasi cha Tsh 5,000/= kwa ajili ya kuhuisha mitaala ya kilimo.
viii. Fedha kiasi cha Tsh 18,000/= kwa ajiri ya kulipia T-shirt inayotumika wakati wa matukio mhimu uwapo chuoni (Inapatikana chuoni), pesa hii inalipwa chuoni kwa mhasibu.

Tafadhali lipa michango yote kwenye akaunti tajwa hapo chini kwani hatupokei pesa tasilimu, isipokuwa risiti ya benki (Bank pay in receipt)

(i) NBC – ELCT IGABIRO TRAINING INSTITUTE OF AGRICULTURE
A/C N0. 027103001001.

(ii) CRDB – ELCT IGABIRO TRAINING INSTITUTE OF AGRICULTURE
A/C N0. 0150216227000

Mahitaji mengine ni kama ifuatavyo;

(i) Sare ya darasani

- Suruali nyeusi na shati jeupe mikono mifupi au mirefu na viatu vyeusi au kahawia kwa wavulana.
- Sketi nyeusi ndefu na shati jeupe mikono mifupi au mirefu na viatu vyeusi au kahawia kwa wasichana.
- Ovalori na Gambuti kwa wanachuo wote wakati wa mafunzo ya vitendo na mitihani.

(ii) Vifaa vya darasani

- Wanachuo wote wanatakiwa kuja na daftari/counter book nane (8) kwa semista, kalamu za risasi na wino, rula, kifutio, mathematical set na pesa kwa ajili ya stationery na kujikimu.
- Kikokotozi (Scientific calculator).

(iii) Vifaa vya bwenini *(kwa mwanachuo wa bweni)*

- Mwanachuo anatakiwa kuja na godoro 2.5`x 6`, shuka mbili, blanket, chandarua na mto.

(iv) Vyombo vya kulia chakula *(kwa mwanachuo wa bweni)*

- Mwanachuo anatakiwa aje na sahani, bakuli, kijiko na kikombe.

(v) Vifaa vya michezo

- Mwanachuo anatakiwa aje na vifaa vya michezo kulingana na aina ya michezo anayopendelea.

(vi) Vifaa vya usafi *(kwa mwanachuo wa bweni)*

- Mwanachuo anatakiwa aje na vifaa vya usafi wa mwili kama vile ndoo/beseni, mswaki, sabuni nk.
- Mfagio wa usafi wa ndani (hard broom)

(vi) Vitendea kazi

- Jembe lenye mpini, fyekeo au kotama.

MUHIMU:-

Mwanachuo anatakiwa kuwa na fedha ya somo la mazoezi kwa vitendo atakayoitumia akiwa nje ya chuo kwa mwezi mmoja . Fedha hiyo ni kati ya

Tsh **200,000/=** hadi **350,000/=** kulingana na uwezo wa mzazi / mlezi / mwajiri kwa ajili ya chakula na malazi. Mazoezi ya vitendo yanafanyika mwanzoni mwa semista ya pili.

Mahali chuo kilipo

Chuo cha mafunzo ya Kilimo na Mifugo **Igabiro** kipo wilayani Muleba – Kagera. Kutoka Muleba mjini ni Kilometa 15 magharibi ukipitia barabara ya Nshamba. Na kutoka Nshamba kufika chuoni ni kilometa 3 kusini mwa Nshamba barabara ya kwenda Kabale upande wa kushoto kuna kibao kinachoonesha chuo kilipo.

Kutoka manisipaa ya Bukoba, pita barabara ya Bukoba – Muleba au Bukoba – Kamachumu kuja Nshamba.

Mara ufikapo chuoni, wasiliana na afisa udahili (Admission Officer) kwa usajili na malazi pamoja na huduma zingine mhimu.

Hakikisha unakuja na fomu ya kujiunga na chuo(joining instruction) wakati wa usajili. Unatakiwa kuripoti chuoni mapema kama tarehe zinavyo elekeza, kushindwa kufanya hivyo inaweza kupelekea kupoteza nafasi hiyo.

Maelekezo ya jumla

- ✓ Masomo yako yatachukua muda wa mwaka mmoja.
- ✓ Lipa ada na michango mingine kwa wakati sahihi ili kuepusha usumbufu kwa mwanachuo na upande wa utawala.
- ✓ Ukiwa chuoni unatakiwa kuzingatia sheria za chuo kama zinavyoelekeza.
- ✓ Hakikisha umeweka utaratibu mzuri wa kazini kwako au nyumbani ili kuepusha ruhusa za mara kwa mara ambazo zitapelekea kupoteza vipindi vya darasani.
- ✓ Hakikisha unakuja na vyeti halali ili kuepusha usumbufu
- ✓ Tengeneza nakala ya fomu ya maelekezo ya kujiunga na umuachie mzazi, mlezi au mwajiri wako kwa ajili ya kurejea maelekezo yaliyomo kama vile utaratibu wa kulipa ada na michango mingine.

…… ……

Saini ya Mwanachuo Tarehe

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
NORTH WERSTEN DIOCESE
IGABIRO TRAINING INSTITUTE OF AGRICUTURE
P. O.BOX 212-MULEBA,
Mobile Phone: 0754756028
Email: igabirotia@yahoo.com and **Website:** www.igabirotia.ac.tz

TO: The Medical Officer

……

……

1. Name……..
2. Age ……..
3. Weight …..……..……
4. Blood Examination: Hemoglobin ……

   Any abnormalities noted …….....
5. Stool Examination……
6. Urinalysis ……
7. T.B. Test (if negative, was immunization given)

   ……
8. Eyes ……..
9. Chest……
10. Abdominal Examination …….…….…….....
11. Spleen ……

    Liver ……..……
12. Any clinic complaints not noted above ……

    Asthma ……

    Headache ……

Signature and stamp

(**Medical Officer)**